ZIJUE HAKI ZA WANAWAKE

SHERIA KATIKA LUGHA RAHISI

KIMETOLEWA NA CHAMA CHA WANASHERIA TANZANIA BARA (TANGANYIKA LAW SOCIETY) KWA UFADHILI WA TAASISI YA LEGAL SERVICE FACILITY (LSF)

JANUARI, 2016

ZIJUE HAKI ZA WANAWAKE

SHERIA KATIKA LUGHA RAHISI

KIMETOLEWA NA CHAMA CHA WANASHERIA TANZANIA BARA (TANGANYIKA LAW SOCIETY) KWA UFADHILI WA TAASISI YA LEGAL SERVICE FACILITY (LSF)

JANUARI, 2016

KIMEANDALIWA NA
Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara (Tanganyika Law Society)
Kiwanja Na. 391, Mtaa wa Chato
Regent Estate, S.L.P 2148
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 2775313 / +255 22 5500002
Nukushi +255 22 2775314
Barua Pepe info@tls.or.tz
Tovuti www.tls.or.tz

© Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara, 2016

Waandishi
- Kaleb Gamaya,
- Mackphason Buberwa
- Stephen Msechu
- Celina Kibasa
- John Mwang'ombola
- Alphonce Gura
- Judith Kapinga

Wahariri
- Magdalena A. Mlolere,
- Stephen Msechu

Kimeandikwa na kuhaririwa chini ya usimamizi wa;

Kamati ya Msaada wa Sheria
- Anna Kulaya-Mwenyekiti
- Butamo Philip
- Daniel Lema
- Donesta Byarugaba
- Fulgence Massawe
- Maria Matui

Kamati ya Utafiti na Machapisho
- Prof. Cyriacus Binamungu
- Dr. Alex Makuklilo
- Dr. Lilian Mongela
- Elifuraha Laltaika
- Madeline Kimei
- Nuhu Mkumbukwa

Yaliyomo

SHUKRANI iv

Utangulizi 1

Mikataba ya Kimataifa inayolinda Haki za Wanawake 1

Maana ya Ubaguzi: 2

Mkataba nyongeza wa Haki za Wanawake Barani Afrika wa mwaka 2003 2

Sheria na Sera za Nchi zinazolinda Haki za Wanawake 3

Baadhi ya Sheria zinazolinda Haki za wanawake Tanzania 5

Mikakati ya Ulinzi wa Haki za Wanawake katika Jamii 7

Baadhi ya mambo yanayokiuka au kuvunja haki za wanawake Tanzania 7

SHUKRANI

Kamati ya Msaada wa Sheria ya Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara inatoa shukrani za pekee kwa wadau mbalimbali kutoka mashirika ya kutoa msaada wa kisheria kwa ushauri wao maridhawa katika kuandaa kijarida hiki cha ***Zijue haki za wanawake***.

Pili, Shukrani ziende kwa Taasisi ya Legal Service Facility (LSF) kwa ufadhili na ushauri wa kipekee katika kuandaa kijarida hiki.

Pia Kamati inatoa shukrani za dhati kwa Baraza la Uongozi la Chama cha Wanasheria chini ya Rais Charles Rwechungura na Sekretariat ya Chama chini ya Kaleb Gamaya kwa rasilimali na ushirikiano waliotoa katika kukamilisha kazi hii muhimu kwa taifa letu inayolenga kukuza uelewa wa sheria miongoni mwa wananchi.

UTANGULIZI

Wanawake na wanaume wana haki sawa. Hata hivyo kutokana na sababu mbalimbali wanawake hawakuweza kufaidi haki zao kama wanaume. Mikataba mbalimbali imepitishwa kuhakikisha wanawake wanafaidi haki sawa na wanaume. Pia kuna sheria mbalimbali za nchi zinazolinda haki za wanawake

Ikumbukwe kuwa mikataba mikuu ya haki za binadamu imeweka kanuni kuu ya kutobaguliwa katika kufaidi haki za binadamu kwa misingi ya jinsi, dini, kabila, rangi, umri, utaifa, na kadhalika. Hii inamaanisha kuwa haki za binadamu zapaswa watu wote wazifaidi bila ubaguzi wa aina yoyote.

Hata hivyo bado baadhi ya makundi ya watu katika jamii hasa wanawake, hawakuweza kupewa nafasi sawa kufaidi haki zao. Ndio maana juhudi zimefanyika na zinaendelea kufanyika katika ngazi ya kimataifa, barani Afrika na hata hapa nchini Tanzania kuhakikisha kwamba haki za wanawake zinalindwa.

Mikataba ya Kimataifa inayolinda Haki za Wanawake

Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake wa Mwaka 1979

Mkataba wa kimataifa wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake au kwa jina jingine unajulikana kama **'Mkataba wa Wanawake'** ndio mkataba mkuu unaolinda haki za wanawake duniani. Mkataba huu ulikubaliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, mwaka 1979 na ulianza kazi tarehe 3 Septemba, 1981. Tanzania imesaini na kuukubali mkataba huu tarehe 19/09/1985.

Mkataba huu umelenga kuhakikisha kuwa wanaume na wanawake wanafaidika kwa usawa na fursa za kiuchumi, kijamii, kitamaduni, kiraia na kisiasa kwa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake

Maana ya Ubaguzi:

Tafsiri ya ubaguzi, kwa mujibu wa mkataba huu, ni tofautisho, au katazo litakalofanywa kwa minajili ya jinsi na kuleta athari kwa wanawake katika kufaidi haki za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Wajibu wa nchi mwanachama

Nchi wanachama kama vile Tanzania zina wajibu wa kulaani aina zote za ubaguzi kufuata sera ya kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake kwa kuahidi yafuatayo:-

- Kuingiza kanuni ya usawa kwa wanawake katika katiba/sheria nyinginezo.
- Kuweka sheria na adhabu pale inapobidi ili kukataza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake.
- Kulinda haki za wanawake kwa msingi ya usawa
- Kufuta sheria zote zinazobagua wanawake
- Kupitisha sheria, kurekebisha, kufuta sheria, mila na desturi zinazochangia kuleta ubaguzi dhidi ya wanawake.

Mkataba nyongeza wa Haki za Wanawake Barani Afrika wa mwaka 2003

Mkataba huu umepitishwa na wakuu wa nchi na serikali za Afrika mwaka 2003 huko Maputo, Msumbiji. Hadi Agosti 2004, ni nchi nne (4) tu za Umoja Afrika zilizoridhia mkataba huu. Tanzania imesaini mkataba huu tarehe 5 Novemba.

Kwa ujumla, mkataba huu ambao pia unajulikana kama “Mkataba wa Maputo” unalinda haki za wanawake wa barani Afrika. Na

mojawapo ya sifa yake kuu ni kutamka wazi kwa mara ya kwanza katika sheria za kimataifa haki za uzazi za wanawake ikiwemo kutoa mimba kama imepatikana kutokana na kubakwa au inamuweka hatarini mwanamke.

Pia mkataba huu nyongeza unapiga marufuku ukeketaji wa wanawake. Kwa ujumla, mkataba wa nyongeza wa haki za wanawake wa Afrika unaweka majukumu kwa nchi na serikali za Afrika kulinda na kutekeleza haki za wanawake katika nchi zao.

Ubaguzi wowote wa kijinsia ni kinyume cha Katiba ya nchi. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) inatamkwa kuwa "binadamu wote ni huru na sawa". Na pia "watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria"

Katiba inakataza sheria kuweka sharti lolote ambalo ni la kibaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake. Ubaguzi unaokatazwa na Katiba unaweza kuwa dhidi ya rangi, kabila, jinsi, utaifa, mahali mtu alipozaliwa au hali ya maisha ya mtu. Kwa maana nyingine, katiba ya nchi inatoa haki sawa kwa wanaume na wanawake nchini Tanzania katika Nyanja zote za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Sheria na Sera za Nchi zinazolinda Haki za Wanawake

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Wanawake na jinsia ya Mwaka 2000
Sera ya maenedeleo ya wanawake ya 2000 (ambayo inachukua nafasi ya sera ya wanawake katika maendeleo ya mwaka 1992) inahusika moja kwa moja na haki za wanawake nchini Tanzania.

Malengo makuu ya sera ni:-

i. Kuweka mazingira muafaka yatakayowezesha wanaweka na wanaume kutekeleza majukumu yao katika jamii kwa kuzingatia mahitaji yao kijinsia.

ii. Kusawazisha mapungufu yanayojitokeza katika ushirikishwaji wa wanawake katika shughuli za maendeleo na

iii. Kuiwezesha jamii ya watanzania kuheshimika imani ya kitaifa ya kuwepo usawa na haki miongoni mwa wananchi bila kuwepo tofauti za kijinsia.

Sera hii inatoa mwelekeo, mikakati na shguhuli mbalimbali za uongozi na maendeleo katika kila sekta na taasisi hapa Tanzania kuhakikisha inazingatia usawa wa kijinsia.

Sera nyingine Zinazotambua Haki za Wanawake

(i) **Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 1997:** Pamoja na mengineyo, sera hii inaweka mikakati ya kulinda na kutetea ajira kwa misingi ya jinsia na usawa. mojawapo ya mikakati hiyo ni kuhakikisha inaondoa sheria za ajira na kazi ambazo ni za kibaguzi dhidi ya wanawake.

(ii) **Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1999:**Sera hii inatambua haki ya kupata elimu bila ubaguzi wa jinsia, rangi, kabila na uwezo wa kiuchumi. Mojawapo ya malengo ya sera hii ni kuhakikisha idadi ya wasichana wanaopata elimu nchini inaongezeka.

Baadhi ya Sheria zinazolinda Haki za wanawake Tanzania

Serikali imepitisha sheria mbalimbali ambazo zinalinda haki za wanawake. Sheria muhimu ni pamoja na:-

(i) **Sheria ya kanuni za adhabu Na. 16:** Sheria hii imekuwepo ili kulinda na kurudisha utu na heshima ya wanawake na watoto. Sheria hii inatoa adhabu kali kwa makosa ya kujamiiana kama vile ukeketaji, ubakaji na udhalilishwaji wa wanawake na watoto wa kile.

(ii) **Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971:** Sheria hii inatoa haki kwa mwanamke aliye katika ndoa. Ufafanuzi zaidi juu ya sheria hii unatolewa kwenye sura inayozungumzia ndoa na mtoto

(iii) **Sheria za Kazi:** Wanawake wanapewa haki ya kuwa na fursa ya kufanya kazi na kulipwa ujira unaostahili. Pia sheria za kazi zinatoa haki ya mwanamke kufaidi mafao ya uzazi.

(iv) **Sheria ya Elimu:** Iinatoa fursa kwa watoto wa kile kupatiwa elimu

(v) **Sheria za Ardhi za mwaka 1999:** Ardhi ni raslimali kubwa ya Watanzania wengi hasa walio vijijini. Kwa muda mrefu wanawake wa Tanzania wamekuwa wakipewa nafasi finyu/ ndogo ya kumiliki ardhi. Mwaka 1999, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha sheria kuu mbili za ardhi ambazo ni Sheria ya Arhi Na. 4/199 na Sheria ya Ardhi ya Kijiji Na. 5/1999.

Mabadiliko makubwa yaliyofanywa na sheria hizi ni kuhakikisha haki ya mwanamke katika umilki, utumiaji na utawala wa ardhi inakuwa sawa na mwanaume bila ubaguzi au upendeleo wowote. Hii inaonekana katika yafuatayo:-

Kwanza, mojawapo ya misingi mikuu ya sheria ya ardhi ni haki sawa kwa wanawake na wanaume katika kupata, kumiliki, kutumia, kuuza na kugawa ardhi kwa kiwango na masharti yale yale bila ubaguzi. Sheria hiyo ya Ardhi inaeleza kuwa sheria yoyote ya kimila itakayokwenda kinyume kwa kuwanyima wanawake, watoto au watu wenye ulemavu uhalali wa kumiliki mali, kutumia au kupata ardhi, basi sheria hiyo ya mila itakuwa batili kwani imevunja sheria mama (katiba) na sheria za nchi.

Pili, mwanamke anatambuliwa kama mmojawapo wa watu wenye haki na sifa ya kuomba kumiliki ardhi sawa sawa kabisa na mwanaume.

Tatu, katika masuala ya usimamizi wa sheria hizi, hasa Sheria ya Ardhi ya Kijijini, wanawake wamepewa nafasi sawa na wanaume ya kushiriki. Mfano, kwenye vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi, kama vile Baraza la Ardhi la Kijiji, sheria inatamka kuwa baraza la Ardhi la jiji litakuwa na wajumbe saba (7) na kati yao angalau watatu lazima wanawake. Kwenye Baraza la Kata ambalo linaundwa na wajumbe wasiopungua wanne na wasiozidi nane, sheria inatamka kuwa wajumbe wanawake wasipungue watatu.

Sheria za Mirathi: zinatoa nafasi kwa wanawake kurithi mali. Hata hivyo kuna mapungufu katika sheria hizi pia.Mifano ya apungufu hayo ni;

- Mjane hana fungu la urithi katika mali iliyoachwa na marehemu mume wake.Bali atatunzwa na watoto wake
- Watoto wa kike wamewekwa katika daraja la tatu ambalo hupata fungu dogo zaidi la urithi kuliko watoto wote.
- Watoto wa kike hawaruhusiwi kurithi ardhi ya ukoo
- Mchango wa mjane katika upatikanaji wa mali za marehemu hautambuliki na hautolewi kabla mali hazijagawanywa kwa warithi wa marehemu.

Mikakati ya Ulinzi wa Haki za Wanawake katika Jamii

Kwa kiwango kikubwa uvunjaji wa haki za wanawake unatokana na mila, desturi na tamaduni. Na kwa kiwango fulani baadhi ya sheria za nchi nazo zinachangia uvunjaji wa haki za wanawake mfano sheria ya ndoa na sheria za mirathi ina vifungu ambavyo havisaidii ulinzi wa wanawake na watoto wa kike.

Baadhi ya mambo yanayokiuka au kuvunja haki za wanawake Tanzania

Mila na Desturi: Kwanza kabisa tuone maana ya maneno 'desturi' na 'mila'. Kwa kifupi neno desturi lina maana ya tabia ya kikundi, watu au kabila fulani, inayotambulika, kukubalika na kufuatwa na watu hao, kikundi hicho au kabila hilo kwa muda mrefu, ambapo mtu akikiuka, anakuwa amekiuka mpangilio.

Mila ni desturi zilizoshamiri au zilizotumika kwa muda mrefu na kukubalika katika jamii husika. Mila hizi zikipata nguvu ya sheria, yaani zikitungiwa sheria, huitwa sheria za kimila.

Makabila mengi hapa nchini yana mila na desturi zao zinazoongoza mienendo ya watu wake katika maisha ya kila siku. Baadhi ya desturi hizo zimekuwa zikikiuka na kuvunja kwa kiwango kikubwa haki ya mwanamke. Tabia kama ukeketaji wa watoto wa kike, kuwanyima wanawake haki ya kurithi mali ya marehemu mume wake au kuwapa cheo cha daraja la tatu watoto wa kike kwenye urithi wa mali ya wazazi wao, kuwanyima haki ya kupata elimu, kuwaoza katika umri mdogo, kuwanyima haki ya kumiliki ardhi n.k ni mifano michache tu ya ukiukaji mkubwa wa haki za wanawake kwa kisingizio cha mila na desturi.

Sheria ya ndoa ya mwaka 1971: Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Sura ya 29 inatoa mwongozo kuhusu haki na wajibu kwa wanandoa, utaratibu kuhusu jukumu la malezi, haki na maslahi ya watoto wa ndoa. n.k

Sheria hii inatambua ndoa za kimila, ndoa za kidini na ndoa za kiserikali zinazofungwa bomani. Hata hivyo sheria hii ina vipengele vinavyokiuka na kuvunja haki ya mtoto wa kike. Kwa mfano sheria inaeleza kuwa wanandoa lazima wawe wametimiza umri unaokubalika kisheria kufunga ndoa (miaka 18 au zaidi). Hata hivyo mwanamke anaweza kuolewa akiwa na umri wa chini ya miaka18 lakini sio chini ya miaka 15 kama atapata idhini ambayo hutolewa na baba na kama hayupo ni mama au kama wote wamefariki idhini itatolewa na mlezi wa binti huyo.Kama wote wamefariki basi hatahitaji idhini. Katika mazingira fulani mahakama pia inaweza kutoa idhini kwa binti kuolewa akiwa na miaka 14 lakini si chini ya hapo ikiwa ataonekana kwa mfano ana mimba. Ndoa chini umri wa miaka 18 ni ndoa ya utotoni na ni ukiukwaji wa haki yamtoto wa kike.

Baadhi ya mikakati wanajamii wanaweza kuitumia kuhamasisha ulinzi wa haki za wanawake katika jamii ni kama ifuatayo

- Kutoa elimu kwa jamii (wanaume, wanawake, viongozi wa kimila, viongozi wa dini, walemavu n.k) kuachana kabisa na mila na desturi zinazomkandamiza, kumuumiza na kumbagua mwanamke.
- Kutoa elimu katika ngazi ya familia na kaya juu ya haki za wanawake
- Elimu hii itolewe kwenye mikutano ya vijiji, mashuleni, masokoni, gulioni, nyumbani, kwenye vikundi vya kuweka na kukopa, vyama vya ushirika n.k
- Kutoa taarifa kwa vyombo husika pale haki za wanawake zinapovunjwa. Vyombo hivi ni pamoja na serikali ya mtaa, polisi, idara ya ustawi wa jamii, asasi za kiraia zinazopinga ukatili dhidi ya wanawake n.k.
- Kushirikisha wanaume kwenye ulinzi wa haki za wanawake

Kumbuka wanawake wanayo haki ya kufaidi matunda ya utu/ubinadamu wao sawa kabisa na wanaume. Baadhi ya mifano ya haki za wanawake ni:-

- haki ya kuishi, uhuru na usalama wa maisha yake
- haki ya kutobaguliwa katika jamii kwa sababu tu ya jinsi yake
- haki ya kutotendewa kinyama au kikatili
- haki ya kumiliki ardhi na/au mali nyingine yeyote inayohamishika na isiyohamishika
- haki ya uhuru wa kutoa na kueleza maoni yake
- haki ya kushiriki katika kutoa maamuzi yahusuyo maisha yake, familia yake na jamii yake
- haki ya kupata elimu

- haki ya kupata fursa sawa ya ajira na kulipwa ujira unaostahiki
- Haki ya afya na afya ya uzazi
- haki ya kupumzika kwa likizo ya uzazi

Kwa kifupi tunaweza kusema kuwa haki za wanawake ni haki za binadamu. Kwani mwanamke anastahili kulindwa na kuheshimiwa utu wake na kufaidi fursa zote zilizoko katika jamii yake kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii.

Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara
Kiwanja Na. 391, Mtaa wa Chato
Regent Estate, S.L.P 2148
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 2775313 /+255 22 5500002
Nukushi: +255 22 2775314
Barua Pepe: info@tls.or.tz
Tovuti: www.tls.or.tz